**JAMHURI YA MUNGANO WA TANZANIA**

**OFISI YA RAIS**

**TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA**

**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA**

**Kumb. Na. BDC/C.30/17/100** **11 Novemba, 2025**

# TANGAZO LA NAFASI ZA KAZI

Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Busega anawatangazia Watanzania wenye sifa kuomba nafasi za kazi **saba (07)** katika Halmashauri hii baada ya kupata kibali kutoka Ofisi ya Rais, Menejimenti ya Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa mchanganuo ufuatao:-

## 1.0 MSAIDIZI MAENDELEO YA JAMII DARAJA LA II - NAFASI 07

### 1.1 MAJUKUMU YA KAZI

i. Kuratibu shughuli zote za Maendeleo ya Jamii kwa kuzingatia jinsia;
ii. Kuraghibisha jamii ngazi ya familia katika kubuni, kupanga, kutekeleza, kusimamia na kutathimini mipango au miradi yao ya maendeleo;
iii. Kuhamasisha kuondokana na mila/desturi potofu na kuwa na mtazamo wa kupenda mabadiriko;
iv. Kuelimisha jamii juu ya kutekeleza masuala ya kijinsia;
v. Kuhamasisha jamii kutumia teknolojia rahisi na sahihi;
vi. Kueleimisha jamii juu ya umuhimu wa kutoa taarifa za matukio mbalimbali kama vile milipuko ya magonjwa, masoko, uzalishaji mali, vyakula, ajira na unyanyasaji wa kijinsia;
vii. Kuhamasisha jamii kujiunga na elimu ya watu wazima;
viii. Kuelimisha jamii kuhusu masuala ya watoto;
ix. Kukusanya, kuchambua, na kuweka takwimu zinazozingatia jinsia zitakazowezesha jamii kupanga mipango ya
x. Kufanya majukumu mengine ambayo atapangiwa na Mwajiri

### 1.1.1 SIFA ZA MWOMBAJI

Kuajiriwa mwenye Astashahada (Certificate) ya Maendeleo ya Jamii kutoka Vyuo vya Maendeleo ya Jamii au Vyuo vingine vinavyotambuliwa na Serikali katika mojawapo wa fani zifuatazo: Maendeleo ya Jamii (Community Development),Sayansi ya Jamii (Sociology, Masomo ya Maendeleo (Development Studies),Mipango na Usimamizi wa Miradi (Project Planning and Management),Jinsia na Maendeleo (Gender and Development),Rural Development, Au fani nyingine zinazofanana na Maendeleo ya Jamii.

### 1.1.2 NGAZI YA MSHAHARA

**TGS B**

### MASHARTI YA JUMLA KWA KAZI.

i. Mwombaji awe Raia wa Tanzania ambaye ana umri usiozidi Miaka 45 na usio chini ya Miaka 18.
ii. Waombaji waambatishe nakala ya Cheti cha Kuzaliwa.
iii. Waombaji waambatishe maelezo binafsi yanayojitosheleza (Detailed CV) yenye anuani na namba za simu za kuaminika pamoja na majina ya Wadhamini (Referees) watatu wa kuaminika pamoja na namba zao za Simu.
iv. Maombi yote yaambatane na nakala za vyeti vya Elimu na taaluma kutoka Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali. Nakala hizo ziwe zimethibitishwa na Wakili au Kamishna wa Viapo.
v. Testimonials, provision results, statement of results, havitakubaliwa
vi. Waombaji wote ambao wamesoma Nje ya Nchi wahakikishe vyeti vyao vinafanyiwa ulinganishi na TCU na NECTA
vii. Waombaji waambatishe (Upload) picha moja Passport size ya hivi karibuni kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira.
viii. Mwombaji kazi ambao tayari ni waajiriwa katika nafasi za kuingilia walioko katika Utumishi wa Umma wasiombe na wanatakiwa kuzingatia maelekezo yaliyo katika Waraka **Na. CAC.45/257/01/D/140 wa tarehe 30 Novemba, 2010.**
ix. Waombaji waliostaafishwa katika Utumishi wa Umma hawaruhusiwi kuomba isipokuwa kama wana Kibali kutoka kwa Katibu Mkuu Kiongozi.
x. Barua ya Maombi iandikwe kwa Kiswahili au Kiingereza
xi. Mwisho wa kutuma maombi ni tarehe **21 Novemba, 2025.**

Barua ya maombi ya kazi iliyosainiwa na mwombaji wa nafasi za kazi ielekezwe kwa;

Mkurugenzi Mtendaji (W),
Halmashauri ya Wilaya ya Busega,
22 Barabara ya Bomani,
S.L.P 157,
**39582 BUSEGA - SIMIYU.**

**MUHIMU: Maombi yote ya kazi yatumwe kwenye Mfumo wa Kielektroniki wa Ajira (Recruitment Portal) kupitia anuani ifuatayo: https://portal.ajira.go.tz/ na si vinginevyo. Anwani hii inapatikana pia kupitia kwenye tovuti ya Sekretarieti ya Ajira kwa kubofya 'Recruitment Portal'.**

xii. Maombi yatakayowasilishwa nje ya utaratibu ulioanishwa katika tangazo hili **HAYATAFIKIRIWA.**

Tangazo hili limetolewa na :

Mkurugenzi Mtendaji (W),
**HALMASHAURI YA WILAYA YA BUSEGA.**